



TANGAZO LA MAENEO YA KUPANGISHA KWA AJILI YA KUTOLEA HUDUMA KWA WANAFUNZI WA CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kinapenda kuutangazia umma kuwa kimetenga maeneo maalumu kwa ajili ya kutoa huduma kwa wanafunzi kama ifuatavyo:

NA.	ENEEO	UKUBWA WA CHUMBA (m ²)	HUDUMA INAYOTAKIWA
1.	Hosteli za Ubungo	Mgahawa unaoweza kuhudumia takribani watu mia moja na themanini (180)	Mgahawa Mdogo wa Chakula
2	Shule Kuu ya Sayansi ya Akua na Teknolojia za Uvuvi (S0AF), Kunduchi	Mgahawa unaoweza kuhudumia takribani watu 100	Mgahawa Mdogo wa Chakula

Kwa tangazo hili, UDSM inawaalika wale wote wenye nia na wanaopenda kutoa huduma hizo kama zilivyoainishwa katika jedwali hapo juu kuomba kutoa huduma hizo. Waombaji wafike Kurugenzi ya Mipango, Maendeleo na Uwekezaji ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam iliyopo Ofisi Namba 228 Jengo la Utawala (Cranford Pratt Building) kwa ajili ya kuchukua fomu za maombi. Waombaji watalipa shilingi elfu kumi tu (TZS 10,000/=) kupitia 'Namba ya Kumbukumbu' ambayo inayopatikana Ofisi Namba 225 kwa Mhasibu wa Kurugenzi ya Mipango, Maendeleo na Uwekezaji.

Mwisho wa kuchukua na kurudisha fomu ni siku ishirini na moja (21) kutoka siku ya kwanza ya tangazo hili.

Tarehe **4 Aprili 2024** itakuwa ni siku ya kutembelea maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya kutolea huduma hizo ambapo saa 4:00 asubuhi waombaji wote wanatakiwa kuwepo katika Hosteli za Ubungo na saa 6:30 Mchana wanatakiwa kuwepo katika Shule Kuu ya Sayansi ya Akua na Teknolojia ya Uvuvi (SoAF), Kunduchi.

Baada ya mchakato wa kupata watoa huduma kukamilika, waombaji wote wataarifiwa juu ya matokeo ya maombi yao kwa njia ya barua.

IMETOLEWA NA
NAIBU MAKAMU MKUU WA CHUO – MIPANGO, FEDHA NA UTAWALA
21.03.2024